# Kumwita Yesu Kwenye Sehemu Ya Tukio

Denham Springs, Louisiana,Amerika
Machi 19, 1964

1 ...tunasoma Neno la Bwana. Katika Injili ya Mathayo, ile-ile sura ya 8, tukianzia na aya ya 23, tunasoma hili.

*Naye alipopanda melini, wanafunzi wake wakamfuata.*

*...tazama, kukawa msukosuko mkuu baharini, hata meli ikafunikizwa na mawimbi: naye alikuwa amelala usingizi.*

*Na wanafunzi wake wakamwendea, wakamwamsha, wakisema, Bwana, tuokoe: tunaangamia.*

*Akawaambia, Mbona mmekuwa waoga, Enyi wa imani haba? Kisha akainuka, na akazikemea pepo na bahari; na kukawa shwari kuu.*

*Lakini wale watu wakamaka, wakisema, Huyu ni mtu wa namna gani, hata pepo na bahari zamtii!*

2 Hebu tuinamishe vichwa vyetu sasa kwa ajili ya maombi. Baba yetu wa Mbinguni, tunayo furaha mno jioni hii kujua kuwa huyu aliye mkuu afanyaye pepo na bahari kumtii Yeye yuko pamoja nasi. Tunashukuru sana kuwa tunao huu ushuhuda mkuu wa Yeye kuwa yu hai leo, na tukijua kuwa Yeye ni wa Milele, kamwe Yeye hawezi kufa. Yeye yu hai milele na milele, na ametuonyesha rehema yake kuu, watoto wa mwanadamu katika siku hizi. Sisi ni watu tulio wahitaji, Bwana, tu wahitaji mno kiasi kwamba hakuna yeyote mwingine angeweza kututimizia mahitaji yetu isipokuwa Wewe. Hivyo tunakutazamia Wewe jioni hii, uje katika kukusanyika kwetu hapa, na ufanye ujulikane Wewe Mwenyewe kwetu kwa kutusamehe dhambi zetu, kuongeza imani yetu, Bwana, na kuponya magonjwa na mateso yetu.

Na tutakapokwenda majumbani mwetu jioni hii, hebu tuwe na furaha, tukisema kama wale wa kutokea Emau, "Je, mioyo yetu haikuwaka ndani Yeye aliposema nasi njiani?" Kwani tunaomba hilo katika Jina Lake. Amina. Mnaweza kuketi.

3 (Mimi ni kama tu Zakayo; haya mambo siku zote ni mafupi mno kwangu.) Nataka kunena nanyi kwa muda mchache tu sasa kabla hatujaombea wagonjwa. Asanteni kwa ushirikiano wenu mzuri, na kuamini katika Roho, jana jioni, tulipokuwa tukinena, nikitumaini kuwa itakuwa ni kumiminika sana kwa baraka Zake.

Siku zote kumbukeni tuko hapa kwa ajili gani, ni kujaribu kuongeza imani yenu katika Uwepo Wake, ili muweze kupokea hilo mnaloliomba. Basi, kwa imani, unaamini.

Sasa, kumbukeni, kila baraka za ukombozi zimekwishanunuliwa. Gharama imelipwa, kuna njia moja pekee ambayo kamwe utaweza kuipokea hiyo: hiyo ni kuiamini na kuikubali. Yeye ni Kuhani Mkuu wa maungamo yetu. Waebrania inasema pale, Waraka wa Waebrania unasema, "Yeye ni Kuhani Mkuu wa maungamo yetu." Kukiri na kuungama ni kitu kile kile, bila shaka. Hivyo sisi… Yeye ni Kuhani Mkuu wa maungamo yetu. Kwa hiyo, Yeye hawezi kutufanyia jambo lolote hadi kwanza tukiri kuwa Yeye amekwishalifanya hilo. Na kisha tunapokiri hilo, basi Yeye ni Kuhani Mkuu, Mpatanishi na anaingia kazini juu ya hilo na kulisahihisha. Hivyo tunaomba, tukimtumainia Mungu jioni hii, katika wema na rehema Zake, kwamba Yeye atatupa wingi wa neema Yake, jioni hii.

Na sasa, kumbukeni, ni lazima mlikubali hilo.

4 Sasa, tunakwenda kuomba kwa ajili ya wagonjwa kabla hatujaondoka, tukiwawekea mikono juu yao, lakini natamani kwamba mngeweza kuwa na imani ya kutosha ili msipaswe kuwa na hiyo. Natamani mngeweza tu kunyosha mikono na kusema, "Bwana Yesu, nakuamini Wewe. Mimi-mimi…" Yeye analiamini Neno.

Mnaona, Mungu ni tofauti na sisi tulivyo. Kama tungalisema mfanye jambo fulani kwa ajili ya kutenda, na hamkuliamini, vema, tungelisema, "Achana nao. Haiwapasi kuliamini." Lakini hilo siyo Mungu, Baba yetu. Yeye ataendelea kufanya jambo fulani lingine ili kukufanya uamini. Yeye anajaribu kushikilia Neno Lake, na Yeye atashikilia Neno Lake. Sasa sababu ya yeye kufanya hayo mambo anayoyafanya sasa, ni kwa

sababu kwamba Yeye aliahidi kuyafanya. Siyo kwamba Yeye anapaswa kufanya hilo, bali Yeye aliahidi kulifanya. Na huo ndio ujasiri wetu-kwamba daima Yeye anashikilia ahadi Yake.

5 Sasa kila mmoja wenu, unapokuwa na wapendwa, walio wagonjwa, na kadhalika, walioketi, kama wao hawawezi… kama yule msichana mdogo hapa, yeye ni mdogo mno, naye yuko katika hali hiyo aliyoko; utakapoamini tu, weka mikono yako juu ya huyo mtoto wakati ibada inaendelea. Wengine, walio na wapendwa, moyoni mwenu mnawawazia; kwa imani wainueni moja kwa moja juu mbele za Mungu, katika maombi.

Sasa, na, kwa hiyo./.. Kisha aminini. Jambo fulani linapotokea, una... Huwezi kujifanya uamini wewe mwenyewe. Wewe, ni kitu fulani, ni ile thamani iliyoko ndani yako. "Imani ni hakika," siyo tu dhana ya kujifanyia. "Ni hakika ya mambo yatarajiwayo, bayana ya mambo unayoyaamini na huyaoni."

Na silaha kamili ya Mkristo sasa, kumbukeni, ni kwa imani. Yote ya Kiungu, upendo, furaha, amani, uvumilivu, wema, unyenyekevu, saburi, mambo yote hayo yasiyoonekana. Hayo ni silaha kamili ya Mkristo. Mkristo wakati wote hutazama mambo ambayo hayaoni, kwa sababu yeye anaitazama ahadi.

6 Hapa muda fulani uliopita, miaka mingi, niliitwa penye sehemu ya tukio, wakati mmoja, hospitalini, ili kumwombea mvulana aliyekuwa anakufa, kwa dondakoo nyeusi. Nimenukuu hili mara nyingi, kwa sababu ni hali maalum sana kwangu. Baba alikuwa ni mtu wa umri wa makamo, na mama. Na huyu kijana alikuwa na kama umri wa miaka kumi na nne, nadhani, na yeye alikuwa mtoto wao wa pekee. Naye alikuwa anakufa, kwa dondakoo nyeusi, na jambo fulani liliutokea moyo wake. Yeye alikuwa amezimia. Na wote walikuwa tu…Yeye tu, ee, kama tu aliyekuwa kufani; nasahau mapigo ya-yake ya moyo yalikuwaje; kule kupumua kulikuwa kwa hali ya chini sana.

Na baba mzee aliendelea kutembelea mikutano, na kuomba, akimwona meneja, na kila mtu. "Njoo uombe! Njoo uombe! Hilo tu, njoo tu hospitalini na uombe."

Meneja akasema, "Mlete mikutanoni."

Yeye akasema, "Hatuwezi kumtoa hospitalini; yeye anakufa." Na kasema, "Kama Ndugu Branham angekuja tu na amwombe Mungu, Mungu angetujalia hilo."

Nikawaza, "Ni imani iliyoje!"

7 Nilikwenda hospitalini, na madaktari hawakuniruhusu niingie.

Wakasema, "Hapana, wewe ni mwanamume aliyeoa, unao watoto." Billy Paul alikuwa mdogo wakati huo. Wakasema, Huwezi kuingia," wakasema, "kwa sababu unaye mtoto."

Nami nikasema, "Sasa, nimeelewa kuwa yule daktari mwenyewe alikuwa Mkatoliki." Nikasema, "Kama padri alitaka kumfanyia kanuni ya mwisho kwa huyu mtoto, kama yeye ni Mkatoliki, je, ungemruhusu aingie?"

Akasema, "Hilo ni tofauti. Padri hana watoto." Unaona? Kasema, "Ungempelekea mtoto wako vijidudu."

Nami nikasema, "Lakini, tazama, bwana, Niache niwajibike. Nitatia saini kwenye karatasi. Nitawajibika. Kama sina imani ya kutosha ya kuingia ndani pale basi kwa ajili ya hilo, sina shughuli ya kuingia ndani, kwanza." Kisha nikasema, "Lakini nitawajibika." Na nikasema, "Liwazie hilo sasa, kama huyo mvulana alikuwa Mkatoliki, na alikuwa anakufa; je, wewe kwa vyovyote ungemzuia padri asimpe kanuni ya mwisho ya kanisa?"

Akasema, "Hapana, singefanya hilo."

Nikasema, "Namaanisha tu kwao kama ambavyo padri hufanya kwa Mkatoliki."

8 Na yeye akasema, "Vema," Na hatimaye akakubali.

Akanivalisha kama anayepingana na Ukatoliki, wa namna fulani, aina zote hizi za vitu juu yangu, na-na kuniingiza ndani pale kwa huyu mvulana mdogo, akiwa anakufa.

Mama na baba walipiga magoti upande ule mwingine. Na niliomba maombi madogo ya kirahisi. "Bwana Yesu, natumaini utamwinua huyu mvulana, juu ya… juu ya msingi wa imani ya baba na mama huyu," na nikaweka mikono yangu juu ya jamaa mdogo. Yeye alikuwa amekuwa hana fahamu kwa kama siku tatu, kama siku tatu, naamini, yeye alikuwa anapumua tu kwa shida. Na nikasimama, nikasema, "Amina." Niliomba kwa

kitambo kidogo, na kusimama.

Na yule baba mzee akamshika mama mikononi mwake, na kusema, "Wazia hilo, mpenzi, mvulana wetu amepona." Hakuna ishara ya hilo hata kidogo. Na wao walikuwa wanakumbatiana tu wao kwa wao, na kumshukuru Bwana.

Na yule mwuguzi mdogo, mtoto mdogo,namaanisha bibiye mdogo, yeye alikuwa na kama umri wa labda miaka kumi na nane, miaka ishirini. Yeye alikuwa na utepe wake wa mwuguzi, na yeye…au yeye alikuwa mwuguzi aliyehitimu. Na yeye akasema, "Bwana, naogopa kwamba wewe huelewi." Akasema, "Huyo mvulana anakufa."

Akasema, "Ee, hapana, huyu mvulana ataishi." Baba alisema.

Na kasema, "Unawezaje kutenda hivyo, na ninii yako…unajua mvulana wako anakufa, penye mwonekano unaodanganya kama huu uliopewa?"

Yeye akasema, "Huo sio mwonekano unaodanganya."

9 Yeye… akasema...

Tazama sasa, naweza…Huenda kuwepo na daktari aliyepo sasa. Mimi sijui hili juu ya udaktari, na vifaa vya maneno ya kidaktari. Walimpa namna fulani ya chombo cha kucheki moyo, na moyo wake ulikuwa unakwenda polepole. Ulikuwa unakwenda polepole kwa muda huo wote. Daktari alisema… Yule mwuguzi akamkumbusha daktari, akasema, "Hilo halikuwahi kujulikana katika historia, kama moyo umekuwa chini kiasi hicho, kwa huo kurejea hali yake tena."

Kamwe sitasahau mtazamo wa yule mwanamume mzee. Jamaa mzee aliye kama baba akatembea na kuweka mkono wake juu ya bega la yule mwuguzi mdogo. Akasema, "Dada," akasema, "unaona, wewe unatazama lile jedwali." Kasema, "Hilo ndilo pekee unalojua, kutazama kwenye hilo. Lakini," akasema, "Mimi naitazama ahadi ya Kiungu."

Yule kijana ni mmishenari katika Afrika sasa, na anao watoto watatu. Unaona? Unaona? Inategemea juu ya kile wewe unachokitazama, unaona. Yeye aliamini.

10 Sasa, hiyo ni imani ile ile, "Kama utakuja uweke mikono Yako juu ya mtoto wangu. Kama Wewe utanena neno, mtumishi wangu..." Unaona, hicho ni kitu fulani ulicho nacho. Wewe-wewe… Basi hiyo haikwa-haikuwa kujifanya. Yule jamaa mzee aliliamini hilo. Yeye alikuwa ameshikilia jambo Fulani. Yule mwanamke aliyegusa vazi Lake. "Kama ninaweza tu kugusa vazi Lake!" Hilo ndilo jambo lenyewe. Ni lazima ushike kwa nguvu hiyo imani, chini katika moyo wako.

Ni kama tu useme... Unajua, wewe mwanamume, kama ni-ni aina sahihi ya mume, hakuna mwanamke ulimwenguni unayempenda kama mke wako. Huenda pakawepo wanawake wengine wanaoweza kuwa wazuri zaidi. Huenda pakawepo wanawake ambao wange-wangekuwa wa-wa-wanawake wenye sura nzuri zaidi, na kadhalika. Lakini jambo fulani, kama kwa kweli unampenda mke wako, kuna jambo fulani ndani pale ambalo huoni jinsi yeye anavyoonekana. Unampenda yeye. Na wewe-wewe hujui ni kwa nini, lakini unampenda.

Na, wanawake, ninyi vivyo hivyo kwa mume wako. Wewe, unapenda. Na ninyi wasichana vijana kwa wapenzi wa kume wenu, wapenzi wa kiume kwenu ninyi mpenzi wa kike. Kama hujakutana na huyo mtu ambaye unajua unampenda, kuna jambo fulani ndani pale unalojua unawapenda wao.

Hhilo ni jambo lile lile lilivyo juu ya imani. Unajua hilo litatukia. Hakuna kivuli, haidhuru ni wangapi wangesema kinyume; bado wewe unaamini jambo lile lile, kwa sababu hiyo ni halisi, imani sahihi iliyo halisi.

Sasa mmwe na hiyo jioni hii, tunaponena juu ya hili somo. Nilinena mno, na nimekuwa katika mikutano kirefu sana sasa, sijawa na utulivu, kwa shida, tangu Krtismasi. Na koo langu linakwaruza kidogo, kutokana na kubadilisha hali ya hewa, na wakati, na kadhalika. Ninataka kunena nanyi jioni hii juu ya somo la, "mwamshe Yesu," au: *Kumwita Yesu Kwenye Sehemu Ya Tukio*.

11 Kutoka kwenye Andiko letu, tunaona kuwa kumekuwa na mkutano mkuu. Yesu alikuwa amekuwa anakwenda huku na huku, akifanya maajabu makuu, akifanya mema siku zote, na pia akifanya kile kilichokuwa kinampendeza Mungu. Siku zote Yeye alimpendeza Mungu, lakini hakujipendeza Mwenyewe, Biblia ilisema. Na tunaona kuwa Yeye alifanya Mwenyewe aweze kujulikana, Yeye alikuwa Nani, kwa njia ya matendo

Yake. Matendo Yake yalimtambulisha Yeye alikuwa Nani. Na nguvu zilikuwa zimemtoka Yeye. Yeye alikuwa akifundisha kwa mifano, siku nzima, na nguvu zilikuwa zimemtoka.

Naye alikuwa… alikuwa anakwenda kuvuka bahari, kukatisha, kule upande mwingine. Kwa kuwa kile Yeye alichokuwa, Yeye-Yeye alijua kulikuwa na kazi kuu mbele, upande ule mwingine. Naye alikuwa amechoka sana. Nguvu zilikuwa zimemtoka, siku nzima, watu walipomgusa Yeye kwa imani yao, kumwamini Yeye, na kadhalika. Na Yeye alikuwa... Nguvu zilikuwa zimemtoka Yeye, naye alikuwa amechoka. Hivyo Yeye alirudi nyuma ya meli na kulala chini juu ya mto, Andiko linatuambia, ili kupumzika kidogo wakati meli inavuka bahari, kuvuka Bahari ya Galilaya, nafasi ya kupumzika kidogo. Wanafunzi Wake wakachukua makasia yao, na kufunga na kuondoka , na kama tu mabaharia wangelifanya. Wao, hiyo ndiyo kazi yao, wengi wao. Wao walikuwa wavuvi kule baharini, na-na wao walijua jinsi ya kuongoza mitumbwi yao. Nao walikuwa wamerejea kwenye kazi yao, wakiwa tu na wakati mkuu wa kufurahi, wakati wa yubile, labda wakizungumza juu ya mambo yaliyokuwa yametukia siku ile.

12 Unajua, kuna jambo fulani kuhusu hilo, kwamba tunapomwona Bwana wetu Yesu akifanya mambo, na kuweza kujua kuwa ni Yeye, kwamba hakuna chochote kingine kingeweza kufanya hilo isipokuwa Yeye, tunaninii tu… Tunapokuwa pamoja, tunaninii tu… Kila mtu anataka kushuhudia. Kila mtu anataka kusema jambo fulani, na wanataka kuzungumza juu ya hilo.

Unaweza kuwa na uamsho kanisani kwako; mchungaji anaweza kunena ujumbe mkuu, au mwinjilisti, au yeyote yule; au unaweza kuona jambo fulani likitukia, au jambo fulani jirani, mtu fulani aliponywa. Majirani wanakusanyika pamoja na kuzungumza juu yake.

"Ni zuri iliyoje! Je, ulikuwepo pale? Ungepaswa ulione hilo. Lilikuwa jambo kuu zaidi sana." Kuna jambo fulani juu ya matendo ya Mungu yanayousisimua moyo wa mwanadamu kuliko kitu kingine chochote kinachotokea. Kuna… Ni tukio tu lisilosahahulika tunapokuja na kukutana na Bwana Yesu na kuona mambo Yeye anayoyafanya, makuu na ya ajabu mno ni njia Zake.

13 Sasa tunaona kuwa tunafurahi juu ya matendo yaliyokwishafanyika katika ile siku ya uamsho, na huenda ningelifananisha na sisi, jioni hii, katika hali ile ile.

Sasa tumeshuhudia tu mojawapo ya miamsho mikuu, naamini, ule ambao ulimwengu uliwahi kuona, katika hii miaka kumi, kumi na tano iliyopita. Imekuwa u-uamsho, siyo tu kama siku za Billy Sunday, au siku za uamsho wa Welsh, au zile siku za-za uamsho wa Wesley, au uamsho wa Moody, au uamsho wa Billy Sunday. Limekuwa jambo lililozagaa ulimwenguni kote, kote ulimwenguni. Ibada kuu za uponyaji na mioto mikuu ya uamsho imeteketeza ilivyowezekana kila kilima kilichoko ulimwenguni. Jioni hii hii, kule katika nchi za Afrika, chini katika China na Japan, Injili hii inahubiriwa, na watu wanaponywa moja kwa moja dakika hii, huko na huko ulimwenguni. Umekuwa mmojawapo wa miamsho mikuu, kwa sababu, naamini, ni mmojawapo wa miamsho wa mwisho ulimwengu huu utaona, uamsho unaozagaa ulimwenguni kote.

14 Lakini sasa, katika miaka michache iliyopita, hiyo imetulia. Huoni shauku katika watu, zamani ilivyokuwa. Nakumbuka kuwa na heshima, kwa njia ya Roho Mtakatifu, kuongoza huo uamsho ulioanza, wakati yule Malaika wa Bwana alipotokea mtoni na kusema hilo, kama miaka mingi iliyopita. Na kwa kuona hilo likitukia, na kuona hilo likiwasha moto mioyo ya wahudumu, kila mahali, miamsho ilitokea. Mbona, ungeweza tu kuingia katika jengo, na watu kusimama kutoka kwenye vitanda vya watoto wachanga na machela, na kuondoka, walioponywa. Hukupasaswa hata kusema neno moja. Ku-kuwa tu pale, ndilo hilo tu lililo tu lililohitajika.

15 Nakumbuka jioni moja katika Vandalia, Illinois. Niliingia mkutanoni, na sikuwa nimekaa mkutanoni zaidi ya dakika tano, na hapakuwepo na mtu mdhaifu pale mahali, kokote. Viti vyenye magurudumu vilitolewa nje na kukusanywa. Vipofu walikuwa wanaona, viziwi na bubu wakinena, na-na hilo tu... Roho wa Bwana alikuwepo,na Yeye aliponya tu hilo kundi lao lote. Sasa hilo ni wakati unaweza kufanya jambo fulani, wakati uamsho unaendelea.

Lakini hebu huo moto wa uamsho uzime, basi unaweza kwa shida... Watu bado ni Wakristo, lakini hawajaamshwa katika huyo Roho, hayo mazingira makuu yanayotenda jambo fulani. Ni kama tu katika karakana ya vyuma, katika duka la mhunzi wa chuma.

Inakupasa kuchukua chuma chenye moto kabla hujakigonga juu ya fuawe. Kama hukufanya hivyo, kamwe hutakinyoosha hicho. Na hilo ndilo linalohitajika kuwa na uamsho, ni kila mtu kuwa chini ya joto la Roho Mtakatifu lililoshusha nguvu za Mungu na uamsho kuendelea. Kisha kuna mikutano ya maombi inayoendelea, mchana na usiku, kila dakika, kila mahali. Mbona, watu hata hawataondoka uwanjani!

16 Nakumbuka katika Jonesboro, Arkansas, wakati nilipanza wangu wa kwanza... kama mkutano wangu wa tatu. Kwanza katika Saint Louis, na kisha kule Corning, na halafu chini kule Jonesboro. Gazeti lilianza, "Watu elfu ishirini na nane katika mkutano." Maili ishirini au thelathini kutokea jijini, ilikuwa ni mahema yaliyowekwa tu. Usingepata nyumba ya shambani ya kulala, hilo jiji dogo la Jonesboro. Na watu wakija kutoka maili, wakiwa na taa za kandili, wakitembea kupita mapori, ku-kupata basi na kuja. Nilikuwa huko nje jangwani jioni moja, nikiomba kabla ibada haijaanza, na niliona bibiye vijana wakija wakiwa na viatu na soksi zao ndefu chini ya mikononi yao. Basi kabla hawajafika chini kule, walisimama na kufuta vumbi miguuni mwao, na kuvaa soksi zao ndefu na-na-na viatu, na-na kwenda mkutanoni.

Na niliwaona wakiwaweka watoto wao walio wagonjwa chini ya gari la zamani la kubebea pamba, na kukaa pale mchana na usiku; wakishiklia makaratasi na nguo za maturubai juu yao, mvua ilipokuwa ikinyesha, dhoruba ikivuma; hawakuondoka sehemu yao, wakisubiri ili tu waingie ndani ya jengo. Hapo ndipo vipofu walikuwa wanaona, viziwi walikuwa wanasikia. Na huduma, jioni hii, iko maili mia mbali na hilo, lakini mioto ya uamsho imezima.

Unaona watu wakitembea juu kule na useme…Unanyoosha tu kidole chako, na kusema, "Vema, je, unaamini, ndugu?" Hivyo tu, yeye alitoka nje na kwenda. Ni hilo tu lililokuwa la kufanyika. Wao waliamini. Uamsho ulikuwa unatembea.

17 Sasa, hawa wanafunzi walikuwa wameona hilo. Na katika hali ya kujitolea wao walikuwa wakiishi kwa furaha-Yesu alipokuwa akipumzika-kwa kile walichokuwa wameona kikifanyika siku ile. Na nafikiri uamsho unafanya jambo kama hilo, kwamba sisi sasa tunaishi tu katika wakati wa ukimya, wakati Yeye anapumzika labda kati ya mikutano, au uamsho na Kuja Kwake. Nasi tunafurahi juu ya hayo mambo tuliyoyaona chini wakati wa huu uamsho, matendo makuu na ya ajabu. Haidhuru ulimwengu unasema nini, bado tunaona hilo lilikwisha fanyika! Hilo ni tamko, hilo ni ukweli, hilo lilikwisha fanyika.

Ni lazima wao wawe walichukua nafasi, wakati meli ilipokuwa ikienda vizuri mno, kuzungumza juu Yake, juu ya matendo Yake, juu ya madai Yake, juu ya Umasihi Wake. Huenda wengi wao wali-… wa hawa wanafunzi, huenda walinena juu ya kile walichoona kikifanyika, wao kwa wao. Kama tu sisi tunavyofanya, wakati wa muda wa uamsho kule Shreveport, wakati wa muda wa uamsho kule-kule kwenye mji mwingine, tutazungumza juu ya hilo.

18 Sasa hivyo ndivyo walivyokuwa wanafanya.

Huenda ilikuwa ni Simoni, kama tulivyozungumza juu yake jana jioni, akisema, "Vema, wakati Andrea aliponiambia kumhusu Yeye, nilitilia mashaka kidogo. Lakini Yeye aliponiambia mimi nilikuwa nani na baba yangu alikuwa nani, hilo liliondoa kule kudhania kote ndani yangu. Ni-niliamini hilo wakati huo."

Huenda ikawa kwamba Filipo labda alisema, baadhi ya hao wengine; huenda ikawa alikuwa Andrea aliyesema. Tulizungumza juu ya bibiye pale kisimani, jana jioni. Huenda walikuwa wanazungumza juu yake, waliposema jambo fulani kama hili:

"Ndugu, mnajua, wakati wangu usio wa kawaida ulikuwa, nili-nilipoondoka kwenda kupata vyakula. Na tukarudi na tulikuwa tumesimama nje kwenye vichaka, na tukamwona Yeye akizungumza na huyu mwanamke mwenye sifa mbaya. Tulifikiri, mioyoni mwetu, 'Vipi kama baadhi ya makuhani wangekuja pale na kuona jambo hili, Bwana wetu akizungumza na huyu mwanamke wa hali hii, wao wangelisema nini kumhusu Yeye?' Na kisha tunakumbuka jinsi tulivyojua, kwamba wao walikuwa na imani na Yeye, kwamba ilikuwa kwa ajili ya kusudi fulani Yeye alikuwa anazungumza na yeye.

"Na kisha Yeye alipomwambia, 'Nenda ukamlete mume wako hapa.' Na yeye akasema, 'Sina mume.' Jinsi mioyo yetu ilivyoruka, kwa sababu tulifikiri kuna wakati mmoja kuna kushindwa. Yesu alikuwa amemwambia huyo mwanamke kuwa alimpasa, aende amlete 'mume' wake, wakati yeye hakuwa na mume. Mnakumbuka mtazamo

tuliokuwa nao juu ya uso wa kila mmoja tuliposhangaa, kuwaza kuwa imani yote tuliyokuwa nayo ndani yake, na ukawa umetoweka kwa ghafla?

"Kisha tunaona, mara Yeye akanena na kusema, 'Umesema kweli, kwani umekuwa na waume watano, na yule uliye naye sasa siyo wako.'"

"Basi yeye alipomtambua Yeye wakati huo kama Masihi, yule Masihi wa Mungu, na kusema pale, kwamba, 'Tunajua kwamba Masihi yu aja. Ni lazima Wewe uwe Nabii, kwani tunajua, Masihi atakapokuja, Yeye atafanya hili.' Na ushuhuda katika huo mji, huo ushuhuda wa huyo mwanamke ulikuwa na ushawishi juu ya watu wa ule mji.

19 "Basi huenda ilikuwa ni Yohana aliyesema, 'Mnajua, nitawaambia lililofanya hilo halisi kwangu, siku ile Yeye alipomega mkate. Sasa, sote tulikuwa na njaa, na Yeye alikuwa ametoka kwenda nyikani, nasi tusingempata, nasi tukakutana na Yeye kule. Na makutano yote ya watu yakaja pale.

Jambo la kwanza mwajua, tulimkuta akisema, 'Wapelekeni mjini, ili wapate chakula.' Na-na Yeye akatuambia 'tuwalishe wao' wakati huo. Na Yeye alikuwa na hizo biskuti tano na samaki wawili wadogo, naye akaumega huo mkate. Na niliangalia mkono Wake alipokuwa anakirudia kipande kingine cha mkate, hiyo biskuti ilikuwa imeongezeka ukubwa tena. Na kisha wakati Yeye aliporudia, akakiweka katika sahani, kisha akarudia, yule samaki alikuwa ameongezeka ukubwa tena. Siyo samaki wa kawaida tu, lakini alikuwa ni samaki aliyepikwa, mnaona, alikwishaongezeka ukubwa tayari."

Yeye alifungulia aina gani ya atomi, ndugu, samaki aliyepikwa, mkate uliookwa, linapita kuongezeka ukubwa? Nasi tunajua Yeye alikuwa Muumba, lakini hapa Yeye anafannya uumbaji wa samaki aliyekwishakupikwa na mkate uliokwishaokwa.

20 Huenda Yoohana alikuwa amesema jambo kama hili. Yeye alisema, "Mnajua, nilipokuwa mvulana mdogo, tuliishi kule chini Yeriko. Nakumbuka mama yangu Myahudi alizoea kunitikisa ili nilale wakati wa adhuhuri; nalala usingizi wangu wa adhuhuri. Nilizoea kumtazama machoni pake, naye angeliniambia habari za Biblia."

Na, mnajua, hilo ni jambo jema kwa mama yeyote kumfanyia mtoto wake. "Mlee mtoto katika njia ipasayo." Ingelikuwa bora kuliko kufungua televisheni na kutazama baadhi ya mambo haya hapa yanayoendelea kwenye televisheni. Ni bora zaidi kama unamsomea habari ya Biblia, kwa sababu inavutia akili yake ndogo.

21 Sasa akasema, "Yeye alizoea… Yeye alizoea kuniambia kuhusu ha-habari ya mwanamke Mshunami akiwa anampokea mvulana wake mdogo akirejea kwenye uhai, kwa njia ya nabii Eliya. Nalipenda hilo. Kisha alizoea kuniambia kuhusu watu wetu wakija kutoka Misri. Na tulikuwa pale pale kwenye Mto Yordani. Na yeye angelinyoosha kidole kukatisha ule mto, na kusema, 'Yohana, waliweka kambi upande ule mwingine tu. Nao walikuwa miaka arobaini katika lile jangwa, na Mungu aliwalisha mana. Nguo zao kamwe hazikwisha. Na Mungu aliwapa mkate, mpya, kila asubuhi.'

"Na ni wangapi wadogo, moyo wa kitoto, nilizoea kusema, 'Mama, je, Mungu alikuwa na matanuru mengi makubwa juu kule angani, na Yeye anaoka mikate hii yote, na kuwaandaa Malaika Zake tayari kushusha mkate wa asubuhi na kuuweka nje kwenye...?'

"'Hapana,' yeye angelisema, 'Yohana, wewe ni mdogo mno kuweza kuelewa. Unaona, Mungu hana matanuru ya kuokea angani. Yeye hahitaji matanuru ya kuokea. Sisi tunapaswa tuwe na matanuru ya kuokea. Lakini Mungu hahitaji hilo, kwa sababu Yeye ni Muumba. Unaona, Yeye hunena tu, na mkate hukaa kwenye... Yeye ni Muumba.'

"Na, ndugu, niliposimama pale leo na kumtazamaYeye akichukua kile kipande cha mkate na kukimega hicho, Naye alichukua kipande kingine, kilikuwa kimeumbwa, nilijua hatukuwa tunamfuata-tunamfuata nabii wa uongo. Yule alikuwa ni Muumba, Mwenyewe, ndani ya Mtu."

Na ninii...

22 Basi huenda wao walikuwa wamejadili mtazamo wa baadhi ya watu; baadhi waliamini, baadhi hawakuamini; na kisha mtazamo Wake juu ya watu. Sasa, mnajua, Ukristo umebadilika mno, katika siku hizi za mwisho. Sasa inakupasa umbembeleze mtu kama mtoto, unawaahidi mengi, unawapa vingi, ili kuwafanya waamini, waje kanisani, na kuwaahidi kuwa watakuwa na washirika bora na kila kitu. Huo sio Ukristo.

Ukristo siyo kuchukuliwa kama mtoto. Ukristo ni kuwa mgumu asiyebadili

msimamo. Sawa. Ni-ni ninii… Ukristo siyo mmea unaooteshwa penye mbolea na unyevunyevu. Mmea unaooteshwa penye mbolea na unyevunyenvu ni mmea uliochanganya mbegu, karibu mara zote. Inakupasa uunyunyizie dawa wakati wote, uondoe wadudu kutoka kwenye huo. Hiyo ni kwa sababu ya udhaifu. Na hivyo ndivyo inavyokupasa kuwafanyia Wakristo wengi, namna ya kuwanyunyizia kwa a-ahadi nyingi. Ninyi, hamhitaji hilo, mmea wa kweli ulio halisi hauhitaji kunyunyiziwa kokote. Wadudu hukaa mbali nao.

23 Ni kama tu leo hii, huyo... mtu anayejaribu kuchukua mambo na kuyapotosha. Mungu, hapo mwanzo, Yeye alisema, "Kila mbegu na izae kwa jinsi yake." Nilikuwa ninasoma katika Reader's Digest hapa, pale wao-wao wanachukua kile tunachoita mhindi uliochanganywa mbegu, na unafanya suke zuri zaidi, kweli, suke kubwa zuri; lakini hilo siyo zuri, hakuna chochote kwenye hili. Nao wanafanya nyanya bora, hata haina ladha kama nyanya, na kufanya, wana kuku sasa ambao hata hawana mabawa. Kuchanganya mbegu!

Mnaona, sasa kumbukeni, unaweza ukawa na mhindi uliochanganywa mbegu, lakini huwezi kurudia kuipanda hiyo mbegu. Haitazaa tena. Itakufa. Kwa nini? Haina uzima ndani yake. Inakupasa uichanganye mbegu kila mara. Kama haitachanganywa, itaendelea tu kuzaliana.

Hilo linaonyesha kuwa mageuzi yenye kuendelea, kulingana na mawazo ya mwanadamu, ni makosa.

24 Unaweza kumchukua fa-farasi jike na punda dume, na kuwazalisha pamoja na upate nyumbu, lakini nyumbu hawezi kuzaliana mwenyewe tena. Imekwisha. Hivyo tu. Yeye amekwisha. Nao wanasema sasa, kwamba katika miaka mingine ishirini, kama hawakuwazuia hawa watu kula hivi vitu vilivyochanganywa mbegu, kama vya mhindi na ngano na vitu ambavyo wanavichanganya mbegu, kwamba, "Hilo linabadilisha huo-huo jinsi ya kusimama kwa wanawake. Wao hawataweza kuwa na watoto, katika miaka ishirini kutoka sasa. Hilo linaua kizazi." Hiyo haina hicho kitu ndani yake.

Mwanadamu hakuufanywa kama zamani alivyokuwa. Mwangalie mwanadamu leo hii. Mbona, wao, zamani walivyokuwa, michezo ya mpira ilikuwa migumu. Sasa inawapasa wavae kofia za chuma; wao wanakufa dazeni kila mwaka, wakigonga juu ya vichwa vyao kama panya, yeye anakufa sasa hivi; hupigana na kila kitu. Mwanadamu amefanywa kutokana na lundo la taka. Ni hilo, na ni kwa sababu ya vitu vilivyochanganywa mbegu, na hilo limechafua mfumo wote wa-wa kuishi kwetu, uchumi wetu wote.

25 Na sasa, huko kuchanganya mbegu kumeingia kanisani, pia. Badala ya kuwa kundi halisi la waamini wa Biblia walio imara, wamelichanganya mbegu hilo kwa njia ya madhehebu. Na wamekuwa na, "Nina *hiki*, nina *kile*; mimi ni wa *hili*, mimi ni wa *lile*." Ni kuchanganya mbegu, na hicho kitu hakiwezi kujizaa tena chenyewe. Tunahitaji Kitabu cha Matendo tena.

Lakini njia pekee utakayofanya jambo hilo ni kurudi kwenye Biblia, na kuwa mbali na baadhi ya hii dini iliyochanganya mbegu. Kuchanganya mbegu, inapasa tufanywe kama mtoto! Hakuna imani, ni kundi tu la wapaka poda, watu wenye tabia ya kike tu, waliolelewa kitoto ndani yake.

Nasema, "Je, wewe ni Mkristo?

"Mimi ni Mmethodisti."

"Je, wewe ni Mkristo?"

"Mimi ni Mpresibiteri."

"Mimi ni Mpentekoste."

Hilo halimaanishi hilo, mbele Zake Mungu.Wewe ni Mkristo kwa sababu umezaliwa katika Roho wa Kristo, na Neno la Mungu linaishi ndani yako.

26 Unajua, siku zote hufurahia farasi aliyechanganya mbegu…Unajua, yeye ana akili. Unaweza-unaweza kumfundisha mambo, kumfanyia mambo, naye atajifunza. Lakini mchukue nyumbu wa kale, huwezi kumfanyia lolote. Yeye ni punda wa kale tu mwenye masikio marefu. Yeye huketi pale, na, ungezungumza na yeye, yeye angetoa masikio yake nje, na "Loo? Loo? Loo?" Unaona, huyo, yeye amechanganya mbegu tu. Uweke akilini, wengi wa hawa waitwao Wakristo, waliochanganya mbegu, dini ya punda.

Unawaambia Yesu Kristo ni yule jana, leo, na hata milele."

Wao wanasema, "Mimi siamini Hilo." Unaona? Na hivyo kamwe hutaweza kumfundisha chochote. Dheheb, hilo limeondoka, hata hivyo.

"Kanisa langu huliamini Hilo hivi."

"Langu huliamini Hilo hivi."

Lakini Neno la Mungu linasema Yeye ni yule jana, leo, na hata milele! Simpendi Mkristo aliyechanganya mbegu. Napenda-napenda ukoo wa farasi. Yeye anajua baba yake alikuwa nani, mama yake alikuwa nani, babu na nyanya walikuwa nani. Yeye anajua vizazi vyote kote huko nyuma. Vivyo hivyo na ukoo wa Mkristo, yeye anajua Baba yake ni nani. Yeye anatoka kwa Mungu; Yeye ni Neno la Mungu, Yeye ni yule yule kama Yeye alivyowahi kuwa. Yeye ni zao halisi la ukoo wa Mungu, Neno la Mungu liko ndani yake, Yesu Kristo akijidhihirisha Mwenyewe.

27 Lakini kwa wasioamini... Yesu alitaka kutikisa kundi la wanyonyaji siku moja, Yeye alikuwa na wengi mno waliokuwa wakimfuata. Yeye alikuwa na wanafunzi Wake. Kisha, Yeye alikuwa na wale sabini, jumuia ya wahudumu. Kisha Yeye alikuwa na kusanyiko, kwa maelfu. Na halafu Yeye alifanya hili tamko, akasema, "Isipokuwa mtakula Damu… mle mwili wa Mwana adamu, na kunywa Damu yake, hamna Uzima ndani yenu."

Sasa unafikiri daktari wa hospitali angesema nini, akiwa ameketi nje katika kusanyiko? Unafikiri mtu mwenye kuwaza kwa busara angefanya, kile tunachoita kuwa na busara? Kamwe yeye hakuelezea hilo. Haikumpasa kulielezea hilo.

"Mbona," daktari angesema, "Achana na huyo Jamaa. Yeye ni mwendawazimu. Yeye… Tutakuwa wanyonya damu ya mwanadamu. Kunywa Damu ya Mtu, kula nyama Yake?"

28 Na kusanyiko, ningewaza kuhani alisema, "Huu ni wakati. Hapa ndipo ambapo tunaingia ndani. Tuondoke! Kamwe hatutahudhuria mmoja mwingine wa hiyo mikutano." Wakaondoka. Kisha, yeye akawaondoa hao wote wamwache Yeye.

Kisha Yeye akageuka na akawaambia hao sabini, Akasema, "Mtasema nini mtakapomwona Mwana adamu akipaa juu Mbinguni Yeye alikotokea?"

Sasa, hao sabini wakasema, "Mwana adamu akipaa juu alikotoka? Mbona, Yeye ametuonyesha pale pale kwenye hori la ng'ombe alikozaliwa. Tunamfahamu mama Yake. Tunaona nguo, nguo za kitoto alizofungiwa. Yeye alizaliwa chini kule katika Bethlehemu ya Yuda. Yeye alilelewa hapa Nazareti. Hao hapo kaka Zake, dada Zake, na hao wote pamoja nasi. Na kisha Yeye anasema, 'Huyu Mwana adamu anapaa juu?'"

Sasa, Yeye hakulielezea hilo, Yeye alilisema tu. Sasa, wao wasingeweza kulielezea, wasingeweza kulielewa katika akili zao.

"Vema," walisema, "hapa ndipo tunapoingia," hivyo wakatoka nje. Hilo ndilo pekee wangeweza kuhimili. Bado wao wanayo makundi hayo hayo. Hilo ni sahihi. Bado tunao.

Tunaona.

29 Kisha Yeye akageuka. Kumbuka, hao wanafunzi wasingeweza kulielezea hilo, wala, lakini wao walikuwa na imani. Basi Yesu aligeuka na akawatazama wale kumi na wawili, na kusema, "Ninyi nanyi mwataka kuondoka?"

Ndipo Petro akasema hayo maneno mashuhuri, "Bwana, twende wapi? Kwani tumeshawishika kabisa, sisi tunajua kuwa Wewe unalo Neno la Uzima, na ni Wewe pekee."

Wao hawakuweza kuelezea jinsi watakavyokula mwili Wake na kuinywa Damu Yake. Wao hawakuweza kuelewa jinsi Yeye atakavyopaa juu kule Yeye alikotoka na kushuka chini, wakati Yeye alikuwa amezaliwa Bethlehemu. Hawakuweza. Lakini, unaona, imani haijui kushindwa. Imetia nanga. Inadumu pale, haidhuru kitu kingine kinasema nini. Inadumu pale. Wao waliwekewa huu Uzima. Na Yeye… Wao walidumu pale.

30 Sasa hao aina mbalimbali. Baadhi waliamini. Baadhi wakasema, "Mtu hakuwahi kunena namna hii."

Baadhi hawakuamini, nao wakasema, "Ee, hilo... tulipaswa kulijadili hilo."

Baadhi walisema, "Mtu hakuwahi kunena kama huyu Mtu. Kuna jambo fulani la

ajabu juu Yake. Kile Yeye asemacho, Yeye anaweza kukitetea."

Vema, wao walisema hilo, unajua, wakasema, "Yeye hasemi kama kuhani. Yeye hasemi kama rabi. Kwani kile Yeye asemacho, Mungu anakitetea. Yeye anakithibitisha kile Yeye alichosema." Loo, jamani!

Huenda ilikuwa kijana Yohana, wakati huo, aliyesema, "Wazia hilo! Tumekuwa Naye pamoja nasi hivi sasa. Ni faraja iliyoje hiyo! Ni usalama ulioje!" Huo unapasa uwe usalama ulioje kwetu!

31 Mimi ni mmishenari, kuzunguka na kuzunguka ulimwenguni. Na nimeona aina zote za dini na aina zote za miungu waliyo nayo, miungu makafiri; Waislamu, Budha, na Sikh, Jain, ee, chochote kile, na miungu makafiri wa makabila. Lakini, kila mmoja wao, hakuna mmojawapo ulio sahihi isipokuwa Ukristo. Kila mmoja wao, waanzilishi wake wamekufa, nao wana kaburi pale yeye alikozikwa. Lakini Ukristo ndio pekee ulio sahihi, kwa sababu Mwanzilishi wetu alikufa, akazikwa, lakini alifufuka tena, na tunaweza kuthibitisha kwamba Yeye yu hai.

Penye kaburi la Mohammed, kwa miaka elfu mbili iliyopita, karibu, amekuwako farasi mweupe, walinzi wanabadilishwa kila baada ya masaa kadha, wakimsubiri Mohammed afufuke kutoka kwa wafu na ampande kwenda ulimwenguni na kuteka.

32 Lakini Yesu amekwishafufuka kutoka kwa wafu, amekuwa juu kwa miaka elfu mbili, na yuko nasi jioni hii.

Na kisha tunapoona hili giza, na kuona wakati wa mwisho, jinsi ilivyo hivi sasa, tukija kwenye masaa tunayoishi, tunapokazana kwenye njia ya kuendeshea mashua ya tanga kufikia boma la maji muhimu ya maisha, pale ambapo bahari zenye dhoruba, na-na hicho chombo kinaweza kuvunjikavunjika wakati wowote. Hizi taa ndogo zinaweza kumulika kupiga picha namna hiyo.

Au, huenda kamwe tusiondoke kwenye hili jengo jioni hii, hata mmoja wetu. Hatujui ni wakati gani mauti inakuja. Ilikuwa jinsi ilivyokuwa kujisikia salama, kwa hao wanafunzi, kule kujua kwamba yule yule Muumba, ambaye alikuwa amejitambulisha kikamilifu kuwa yule Mtu, alikuwa anasafiri baharini pamoja nao. Ni wazo la baraka iliyoje, ni tumaini la baraka iliyoje, ni hakika iliyoje, katika saa hii ya giza penye mwisho wa historia ya ulimwengu, kujua Muumba yu nasi kwenye boma kuu la maji muhimu ya maisha, tumefanikiwa salama ndani! Mabomu, chochote kinachoweza kuja, hebu yaendelee, yalipuke, yapasuke, chochote wanachotaka, haifanyi tofauti kwangu, mimi ninasafiri baharini na Muumba. Ni usalama ulioje, ninaposafiri kwenye haya maji!

33 Sasa tunaponena, tukizungumza juu Yake, kuhusu yale mambo makuu Yeye aliyokwishafanya. Baada ya karamu ya uamsho, labda Yesu alikuwa anapumzika kama Yeye alivyo, nilisema, kati ya miamsho. Na sisi… wao walikuwa wametambulishwa kwa uwazi kuwa Yeye alikuwa Nani. Watu walijua Yeye alikuwa Nani, wa hao ambao Yeye alikuwa anawapofusha. Lakini wale ambao walikuwa wameshikilia Maandiko, kwa sababu wao walijua Maandiko…Neno la Mungu lilikuwa limetolewa, fungu, kwa kila kizazi, na hiyo ahadi ya hicho kipindi ilipasa itmie. Na Yeye alitimiza kabisa kile kilichopaswa kufanyika katika wakati wa Masihi. Yeye alikuwa na kila sifa. Kisha sisi…yeye alihakikishiwa kuwa Yeye alikuwa yule Mtu.

Lakini, mnaona, Yeye alikuwa wa kawaida mno. Yeye hakuvalia kama kuhani. Yeye alikuwa, hapana, hakuwa na elimu kama-kama kile ambacho tungekiita elimu. Hatuna kumbukumbu Yake hata ya kwenda shule. Lakini kulikuwa na kitu fulani juu Yake kilichokuwa tofauti.

Na kisha Yeye aliwaalika hao, wakati wao hawakuweza kuelewa, akasema, "Chunguzeni Maandiko, kwani mnadhani ndani Yake mna Uzima wa Milele, na hicho ndicho kitu kinachonishuhudia Mimi. Yanaelezea Mimi ni Nani."

34 Na sasa, kumbukeni, wao walikuwa na yote aliyokuwa nayo huyu moyoni mwao na walikuwa wakiwaza juu ya haya mambo.

Na walipokuwa wakisafiri baharini, jinsi ambavyo wao wangekuwa kama watoto, maadam Yeye alikuwa ndani ya meli pamoja nao. Sasa, rafiki, hilo linapaswa kutufanyia nini! Yesu Kristo yule yule aliyetambulika, Muumba yule yule, Mungu yule yule, yuko pamoja nasi jioni hii. Ni usalama u-ulioje, ni kujisikia iliyoje, kule kujua kwamba Uwepo Wake uko hapa.

Sasa tunaona, pale pale walipokuwa na huu wakati mkuu, ghafla, tatizo likainuka. Meli ikasukasuka, matanga yakalipuka, maji yakajaa mtumbwi. Matumaini yote ya kunusurika yalikuwa yameondoka.

Sasa, je, hilo si la ajabu, kama tu ilivyo sasa, tunapofikia mwisho sasa, je, hilo si la ajabu? Tunaweza kuzungumza kuhusu jinsi Yeye alivyo mkuu; tunaweza kuelezea jinsi Yeye alivyo mkuu, katika kanisa letu tunaposhuhudia; tunawaambia wa-wafanyakazi wetu, waajiri, jinsi Yeye alivyo mkuu; tunaelezea watu barabarani jinsi Yeye alivyo mkuu, tatizo linaposhambulia, tunafadhaika. Mnaona? Tunaninii tu…Mnaona? Yale mambo tuliyomwona Yeye akifanya, yale mambo ambayo tunajua Yeye hufanya; na hebu achia tu ugonjwa kidogo, au tatizo dogo lishambulie nyumba, tazama kinachotukia; yote yamekwenda vipande vipande, matumaini yo-yote yanaondoka. Ingawa wao wamemwona Yeye akifanya mambo mengi; yote yamesahaulika tatizo linashambulia.

35 Kama sasa, tumeona uamsho mkuu, tunayo historia ya miamsho mingine mikuu, tumekuwa na Uwepo Wake, tunajua haya mambo, na wakati mwingine matatizo huja ambayo hatuwezi kuyaondoa.

Wao... Kwa mfano kama sasa, tuna tatizo katika makanisa yetu sasa. Tunayo matatizo ya kidhehebu, mabishano katika makanisa yetu. Hatujui nini kinakwenda kutokea. Tunaona jambo fulani kuu likiumbika juu kule. Sisi sote waaminio tunaona katika Biblia jambo fulani linalojiandaa kutokea. Hakuna mtu yeyote isipokuwa hicho tunachojua hilo.

Na makanisa yote yataletwa katika Baraza la Makanisa. Kisha, utakapofanya jambo hilo, unakwenda kupoteza fundisho lako kuu la kiinjilisti la Biblia. Na Wapentekoste wanakubaliana nalo, wanakwenda moja kwa moja ndani yake, kama nguruwe anayekwenda kwenye machinjio yake, hiyo ni sahihi, baraza la makanisa. Viongozi wengi wakuu wa Pentekoste wanaafikiana nao.

Nawambieni kamwe usiingize shingo yako katika kitu kama hicho. Hicho ndicho hasa Biblia ilisema kingetukia. Huyo hapo yule mnyama na ile alama, na, kikamilifu, kila kitu kimewekwa katika utaratibu, na tunaona hili na tunashangaa matokeo yake yatakuwa nini.

36 Tatizo likaingia. Na wao wakasahau kwamba Yule Yule ambaye walikuwa wanazungumza kumhusu, yule yule Muumba, alikuwa ndani ya mtumbwi pamoja nao. Sasa unasema, "Kama ningeweza kuwaza hilo!" Vema, kumbukeni, bado tunaye Yeye, kwa sababu Yeye ni Neno, siku zote.

Katika Yohana 1:1, kama tulivyonena jana jioni, "Yeye alikuwa Neno; naye Neno alifanyika mwili na kukaa miongoni mwetu." Na bado tunalo Neno Lake linalotuongoza kwenye mawazo Yake na matendo Yake kwa ajili ya siku hii. Mnaona? Ninii… Siyo mawazo ya Musa aliyokuwa nayo katika siku yake, siyo mawazo ya wale wanafunzi, siyo mawazo ya Luther, au Wesley, au kipindi cha Pentekoste, au chochote cha hivyo. Tunayo Biblia hapa inayotuambia juu ya kile kitakachotukia hivi sasa. Mnaona?Tunaona uamsho wa Pentekoste katika Biblia, Lutherani, na vipindi vyote hivyo vya kanisa. Tuliona hivyo vyote. Lakini pia tunalo Andiko hapa linalotuambia nini kinakwenda kuwa sasa. Na huyo ni Mungu, Mungu akifasiri Neno lake Mwenyewe kwa kipindi hiki tunachoishi. Yeye anajifasiria Mwenyewe. Na, bado, tunafadhaika. Tusifadhaike.

37 Wanafunzi Wake wakati mwingine waliingia katika matatizo kimwili ambayo hawawezi kuyaondoa, kama ugonjwa, saratani, kadhalika, ambayo madaktari hawawezi, hawajui nini cha kufanya juu ya hilo. Sisi, kama wao, tunasahahu ni Nani aliye ndani ya meli. Wao wangepaswa kujua kuwa Yeye alijua mambo haya yote.

Yeye alijua hayo yalikuwa yanakwenda kutukia. Yeye alikuwa ninii… Yeye alijua mambo yote, hivyo Yeye alijua hili lilikuwa linakwenda kutukia. Lilikuwa linakwenda kutukia kwao. Kwa nini yeye alikuwa anaruhusu hilo litukie? Yeye alipoingia ndani ya meli, alijua kuwa hilo linakwenda kutukia. Yeye anajua kuwa ilitupasa tukutane na hali hii, na Yeye alitangulia kutuambia hapa katika Biblia ingekuwa namna hiyo. Sasa Yeye alikuwa anafanya nini? Akijaribu imani yao.

38 Kwa nini Yeye aliruhusu mwanamke m-m-mzuri, mdogo, aliyeonekana kama mama aketi katika kiti chenye magurudumu, namna hiyo? Kwa nini Yeye aliruhusu jamaa vijana wazuri hapa, hawa wanaume vijana walioketi hapa katika hivi viti vyenye magurumu, akina bibiye, na kadhalika? Kwa nini Yeye aliruhusu? Na, bado, wanaweza

wakalemaa, waishi tu maisha ya kawaida. Lakini huenda pakawepo baadhi walioketi hapa wenye tatizo la moyo, na, kama Mungu hakuponyi, unaweza ukawa umekufa kabla ya asubuhi. Hiyo ni sahihi. Yeye alijua hilo lilikuwa litokee.

Huenda hilo limefanyika kuijaribu imani yetu. Hiyo ndiyo sababu hilo lilifanyika kwao. Yeye alisema hivyo. Mnaona? Vivyo hivyo sasa. Yeye alikuwa amedhihirisha Yeye alikuwa Nani, kwa Maneno na ishara alizodhihirisha miongoni, kwamba Yeye alithibitishwa, Masihi aliyepakwa mafuta aliyekuwa aje. Na Yeye amedhihirisha miongoni mwetu, kwa njia ya Ubatizo wa Roho Mtakatifu na kurejeshwa kwa mambo ambayo Yeye aliahidi katika siku hii, ambayo Yeye angelifanya. Yeye amethibitisha kuwa Yeye yuko hapa. Yeye anathibitisha kuwa Yeye ni yule jana, leo, na hata milele. Na kuona jinsi ilivyo rahisi tunaweza kufadhaika penye kitu kidogo? Kamwe tusingeruhusu hilo litokee. Hapana.

Yeye alisema, "Kama siyatendi matendo yaliyoandikwa juu Yangu, basi msiniamini Mimi." Na kama Kanisa, kama Roho Mtakatifu leo, hatendi mambo ambayo alipaswa kutenda kwa ajili ya saa hii, basi msiuamini Ujumbe; mnayo haki ya kutokuamini Hilo.

39 Lakini Yeye aliahidi kuwa mambo haya, Yeye anayoyafanya hivi sasa yatatukia moja kwa moja penye huu wakati. Hivyo hilo linapaswa kutufanya tujisikie salama.

Tuseme, "Ninakwenda kwenye mkutano. Roho Mtakatifu mkuu, nafahamu, yuko juu kule akifunua siri za mioyo ya watu." Hilo ndilo kabisa Yeye alilosema angefanya Yeye atakapofunuliwa katika siku za mwisho. Yesu Kristo alisema, Mwenyewe, kwamba hilo ndilo hasa Yeye angefanya.

Na Yeye alisema, "Ulimwengu utakuwa katika hali kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma." Hapo ndipo tu ulipo sasa. Yeye alisema, "Makanisa yangetengana, kama tu yalivyokuwa wakati ule," Lutu, vuguvugu, chini katika Babeli, au chini katika Sodoma, na Wasodoma. Yeye alisema, "Abrahamu, mteule, kundi lililoitwa watoke," na Yeye alimtuma mjumbe kwa kundi teule. Na yeye alituma wajumbe wawili chini kwao, ikiwakilisha kila moja. Na hilo ndilo tu Yeye alilofanya, hata kwa kila jina, kila tendo, kila hatua, kila kitu kikamilifu tu, kila ishara, kila udhihirisho, hivyo hivyo tu kabisa. Yeye alisema hilo lingetukia. Sasa tuna hofu juu ya nini? Mambo haya yapo kwa ajili yetu? Yeye anatujaribu, aone kile tutafanya kuhusu hilo.

Angalieni.

40 Yeye aliwaambia, akasema, "Sasa, kama hamwezi kuniamini Mimi, aminini matendo niyatendayo; haya yananishuhudia Mimi ni Nani." Walipaswa wawe wanajua hilo, lakini hawakujua. Yeye alikuwa Mungu, Aliyeumba, Muumba wa pepo na bahari. Kama Yeye aliweza kuumba pepo na bahari, je, Yeye asingeweza zaidi kuzifanya zitii Neno lake? Kama Yeye aliumba kila kitu, je, Yeye hawezi kufanya kila kitu kitii?

Hebu tukumbuke, pia, Yeye aliumba miili yetu, hiyo pia itapasa kutii Neno Lake. "Vema," unasema, "kama tu ningekuwa na hakika na hilo." Vema, tuna hakika na hilo. Yeye yuko hapa kuthibitisha hilo. Inapaswa itii Hilo. Kumbukeni. Yaya anapaswa... Wakati tunapomwagwa, si chochote isipokuwa labda kijiko kilichojaa majivu, Yeye aliahidi kufufua hayo majivu. Yeye aliahidi kuyafufua hayo. Huo mwili inapasa umtii Yeye. Na hiyo ni wakati tunapokufa, tu hakika kuwa tutafufuliwa, kwa sababu Yeye aliahidi angelifanya hilo. Na ahadi Yake ni Neno lake, na tunaamini. Je, mnaamini katika ufufuo wa mwili? [Kusanyiko linasema, "Amina."-Mh.] Hakika. Kama huamini, wewe siyo Mkristo. Hivyo tunaamini kuwa Yeye atatufufua penye siku za mwisho. Yeye aliahidi kufanya hilo. Na hicho ni nini? Hilo ni Neno Lake. Hapo ndipo tunasalimisha kila kitu tulicho nacho, moja kwa moja juu ya hilo Neno.

41 Na kisha inapofikia kwenye wakati ambao tunaona Neno likitambulishwa, kuwa pamoja nasi; basi tunakuwa kama wanafunzi, katika hali nyingine wakati wao walipokuwa nje huko baharini, na-na walikuwa wanakaribia kuzama tena, katika tukio lingine. Nao walimwona Yesu akija akitembea juu ya maji, nao wakapata hofu.

Walisema, "Ni kivuli. Ni utisho." Waliogopa hicho kilikuwa roho, nao wakalia kwa woga. Kitu pekee ambacho kingewasaidia, walikihofia. Na ni hivyo leo hii, kitu kile kile ambacho kinaweza kusaidia watu, wanakiogopa. Yeye alisema, "Msiogope. Ni Mimi."

Yeye ananena. Mngejuaje ilikuwa ni Yeye? Yeye anatambulika kwa Neno lake. Hiyo ndiyo njia Yeye alitambulika mara ya kwanza. Hivyo ndivyo Yeye anatambulika kila wakati, kwa Neno lake. Angalieni.

42 Baada ya hawa wanafu-… wanafunzi walipojikuta wenyewe mwishoni, lazima hilo liliwafanya baadhi yao wang'amue kuwa Muumba bado alikuwa pamoja nao. Natumaini hilo linafanya hilo kwetu, jioni hii, kwani Waebrania 13:8 inasema Yeye ni yule yule.

Kisha wao walifanya nini? Walimwamsha Yesu. "Nenda kamwamshe Yesu. Mwamshe Yeye, mwite Yeye aje kwenye sehemu ya tukio!" Yeye anaitwa kirahisi mno. Walikuwa wameona, waliona mambo mengi mno ambayo Mungu alikuwa ametenda, na-na-na Maneno yakimthibitisha Yeye. Vivyo hivyo nasi. Na yeye ahakuwa mgumu kuitwa katika kutenda. Walimwamsha Yeye, na kusema, "Je, Wewe... hujali Wewe kwamba tunaangamia?"

Unasema, "Tunawezaje kuwa na hakika juu ya hili? Je, unaweza kuthibitisha hilo?"

Yohana 14:12, Yesu alisema, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo mimi, yeye naye atazifanya pia." Hilo ni sahihi. Imani yetu ikimlete Kristo katika uwepo wetu.

43 Yeye alisema katika-katika Luka, sura ya 17, "Katika siku za mwisho wakati Mwana adamu anapofunuliwa, itakuwa kama wakati wa Sodoma na Gomora." Tunaona hilo likitokea. Yeye alisema, kabla huo wakati haujatokea, katika Malaki 4, kwamba, "Kutakuwako na Ujumbe utakaokuja ambao ungelirejesha watu kwenye Imani ya kwanza ambayo ilitolewa mara moja kwa watu." Siku zote mpango wa Mungu ni kufanya hilo. Na kisha waovu watakuwa majivu, na wenye haki watatembea juu ya miguu yao. Tunaona haya yote yakiahidiwa. Yeye anakusubiri sasa hivi, wewe, wewe, kila mmoja wenu, umwite Yeye penye sehemu ya tukio. Kumwita Yeye kwenye sehemu ya tukio! Pale ambapo Yeye anataka kuwa, anaita kwenye tukio la tendo.

Tazama wewe unapomwita penye sehemu ya tukio... Hivyo basi tungesema, "Hebu tumwamshe Yeye." Kisha, tumwite Yeye ahakikishe Neno Lake na kile-kile kitu alichoahidi kufanya, jinsi ambavyo Yeye angefanya. Sisi tungejua, katika ufunuo wa Yesu Kristo katika siku za mwisho, itakuwa kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma. Yeye aliahidi huo ufunuo kwa Kanisa, yeye atakapofunuliwa. Hivyo usitie shaka na kuogopa, yeye ni yule jana, leo, na hata milele.

44 Nilimsikia mwanamke mmoja, wakati mmoja, nilipokuwa nikizungumza kumhusu Yeye kuwa ni mkuu mno. Yeye akasema, "Kuna jambo moja nililo nalo dhidi ya kufundisha kwako, Bwana Branham."

Nikasema, "Vema, asante, kama unalo tu jambo moja." Nikasema, "Natumaini Mungu huliona tu hilo namna hiyo."

Na yeye akasema, "Vema, unamjivunia Yesu mno."

Nikasema, "Natumaini kwamba hicho ndicho kitu pekee kilicho dhidi yangu." Na-na nikasema, "Simjivunii Yeye vya kutosha."

Akasema, "Ee, ndiyo, unafanya hivyo." Kasema, "Unamfanya Yeye UMungu." Ilikuwa ni mwanamke ambaye hakuamini kuwa Yesu alikuwa Mungu. Yeye alikuwa wa sayansi Mkristo. Na akasema, "Unamfanya Yeye-unamfanya Yeye U Mungu, unamfanya Yeye kuwa Mungu."

Nikasema, "Ama Yeye ni Mungu, ama mdanganyifu mkuu zaidi ulimwengu uliowahi kumjua." Nikasema, "Yeye..."

Kasema, "Vema, naweza kukuthibitishia, kwa Biblia yako, kwamba Yeye hakuwa. Yeye alikuwa tu nabii wa kawaida."

Nikasema, "Yeye alikuwa nabii, kwa kweli, lakini Yeye alikuwa Mungu, pia."

Kasema, "Yeye alikuwa mwanadamu na alipatwa na mauti."

Na nikasema, "Hiyo ni kweli, pia."

Akasema, "Akiwa njiani kwenda kumfufua Lazaro kutoka kaburini, Mtakatifu Yohana sura ya 11, akasema, Biblia ilisema, 'Yesu alilia.'"

Nikasema, "Hiyo ni kweli."

Akasema, "Vema, hilo linathibitisha kuwa Yeye asingeweza kuwa Aliye wa Kiungu, na kulia."

45 Nikasema, "Loo, jamani, bibiye, huo ndio ubishi wako?" Nikasema, "Huo ni dhaifu." Akasema… Nikasema, "Kweli, Yeye alikuwa Mtu alipokuwa akilia; lakini wakati yeye alipoweka mwili Wake mdogo katika kutenda, akavuta nyuma mabega Yake madogo na

kusema, 'Lazaro, njoo huku,' na mtu ambaye alikuwa amekufa siku nne, na alikuwa anaoza kaburini, akasimama kwa miguu yake na kuishi tena, huyo alikuwa zaidi ya mwanadamu. Huyo alikuwa Mungu."

46 Yeye alikuwa mwanadamu, nje hapa katika huu mtumbwi usiku ule, Yeye alipokuwa baharini, wakati mapepo ya bahari elfu kumi yalipoapa yangemzamisha Yeye. Huo mtumbwi mdogo wa zamani ulisukwasukwa huku na huku kama kifuniko cha chupa nje huko kwenye bahari yenye tufani. Yeye alikuwa mwanadamu, alichoka, akiwa amelala. Lakini wao walipomwamsha Yeye na kumwita kwenye sehemu ya tukio, Yeye aliweka mguu mmoja juu ya kamba iliyo katikati ya tanga la chombo na kutazama juu, na kusema, "Amani, utulie," na pepo na mawimbi vikamtii Yeye. Huyo alikuwa zaidi ya mwanadamu. Huyo alikuwa Mungu.

Yeye alikuwa mwanadamu aliposhuka kutoka mlimani, mwenye njaa, akiangalia juu ya mti kutafuta kitu cha kula. Yeye alikuwa mwanadamu Yeye alipokuwa na njaa. Lakini Yeye alipochukua mikate mitano na samaki wawili, na kuwalisha elfu tano, huyo alikuwa zaidi ya mwanadamu. Huyo alikuwa Mungu ndani ya huyo mwanadamu.

Mtu ambaye amefikia kamwe kuwa wa thamani ndogo, amekuwa watu walioliamini hilo. Sawa. Washairi na wengine waliliamini hilo, kwamba Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akijipatanisha Mwenyewe na ulimwengu.

47 Na sasa Kristo yuko katika Kanisa, akiwapatanisha watu na Mungu. Yeye aliahidi kufanya hilo.

Imekuwa imeandikwa, kwamba, "Yeye ni yule jana, leo, na hata milele." Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."-Mh.] Naliamini hilo kwa moyo wangu wote, kwamba Yeye anasubiri tu sasa aitwe kwenye sehemu ya tukio.

Sasa kitu pekee kinachoweza kumwita Yeye kwenye sehemu ya tukio, ni sisi kumwamsha Yeye ndani yetu wenyewe, tumwite Yeye kwenye sehemu ya tukio.

48 Yeye ni karama kuu zaidi ya zote ambayo Mungu aliwahi kuupa ulimwengu. "Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe pekee; yeyote amwaminiye Yeye asipotee; awe na Uzima wa Milele." Mtazame Mungu na karama Yake.

Sasa, watu walitumia karama ya Mungu. Mwanamke mdogo, wakati mmoja, yeye aliliamini hilo, kwamba Yeye alikuwa udhihirisho wa Mungu katika mwili. Naye akasema, "Kama nikigusa vazi Lake, -nitafanywa kuwa mzima." Sasa, yeye aligusa vazi lake.

Na Yeye akageuka, na kusema, "Ni nani aliyenigusa Mimi? Mnaona, nguvu, uwezo umenitoka kwangu Mimi." Mwanamke huyo akagusa vazi lake. Hiyo ilikuwa yeye akitumia karama ya Mungu. Unaona? Yeye alipata udhaifu kutokana na hilo.

Lakini Yeye alipoondoka nyumbani kwa Lazaro... Kumbukeni, Mtakatifu (Yohana 5: 19), Yesu alisema, "Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kufanya lolote Mwenyewe, isipokuwa kile Yeye aonacho Baba akitenda." Kumbukeni, Yesu Kristo kamwe hakutenda muujiza mmoja, kamwe hakutenda lolote katika hali ya kimiujiza, hadi kwanza Yeye alipoona ono juu ya kile cha kutenda.

Ni wangapi wanaamini hilo kuwa ni ukweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."-Mh.] Yohana 5, "Amin, siyo kile ninachosikia, siyo kile mtu fulani anachoniambia Mimi; kile nionacho Baba akitenda, ndicho Mwana atendacho pia."

Sasa kama hilo sivyo, basi hayo Maandiko mengine hayako hivyo. "Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno lolote Mwenyewe; ila lile ambalo amwona Baba analitenda, ndilo atendalo Mwana, ndiyo ayatendayo Mwana vile vile. Baba anatenda kazi, na Mimi ninatenda kazi hata sasa." Katika maneno mengine, Yeye alitenda tu, alitenda kile Mungu alichomwambia Yeye atende.

49 Sasa, kumbukeni, wakati Yeye alipoondoka nyumbani kwa Lazaro, alikuwa ameondoka kwa siku kadha. Lazaro aliugua, nao wakamtumia habari Yeye. Yeye hakwenda. Siku mbili baadaye, lazaro aliugua zaidi. Hivyo wakamtumia Yeye habari tena, bado Yeye hakwenda. Kisha wakati ufaao, Baba alikuwa amemwonyesha Yeye kile kingetukia, Lazaro alikufa. Na Yeye akageuka, wakati Lazaro alipokufa, akasema, "Lazaro amekufa, na nafurahi kwa ajili yenu kwamba sikuwa pale." Wangekuwa wanamsubiri Yeye amwombee, na kadhalika. Yeye alitenda tu kile Mungu alichomwambia atende, kile Yeye alichoona, ono. Unaona, Yeye alikuwa ameona ono juu ya kile cha kutenda. "Lakini nakwenda kumwamsha yeye." Loo! Hilo ndilo jambo

lenyewe.

Mtazame Martha akija kumwona Yeye. Alisema, "Bwana, kama Wewe ungalikuwepo hapa, ndugu yangu asingalikufa. Lakini lolote umwombalo Mungu, Mungu atakupa Wewe hilo." Unaona? Yeye alijua kile Yeye alikuwa anakwenda kufanya.

Mtazame Yeye penye kaburi la Lazaro. Alisema, "Baba, nakushukuru, Wewe umekwishanisikia, lakini nimesema tu hilo kwa ajili ya hawa waliosimama hapa." "Lazaro, njoo huku!" Na Lazaro akafufuka kutoka kwa wafu. Sasa, kamwe Yeye hakusema lolote kuhusu kuwa mdhaifu pale. Huyo alikuwa Mungu akitumia karama Yake. Na watu wakitumia karama ya Mungu walikuwa tofauti. Kwani, Yeye alikuwa Neno. "Na Neno ni kali kuliko upanga ukatao kuwili," Biblia inasema, "na hutambua mawazo na makusudio ya moyo." Hilo huthibitisha kuwa Mungu yuko miongoni mwa watu. Ndiyo. Hebu tuliamini hilo. Yeye yuko tayari, kulingana na Neno lake, kuitwa kwenye sehemu ya tukio, jioni hii.

50 Ni wangapi walioko hapa ni wagonjwa na wahitaji, inueni juu mikono yenu. Hebu tuone mikono yenu,, ni wangapi ni wagonjwa na wahitaji, kokote. Vema, kitu pekee Yeye anachokisubiri ni kuitwa kwenye sehemu ya tukio. Mwombe tu yeye.

Sasa vipi kama Yeye alikuwa amesimama hapa akiwa na hii suti aliyonipa Yeye, na wewe unakuja mbele Yake na kusema, "Bwana Yesu, nataka Wewe uniponye," unajua kile Yeye angesema? "Nimekwishafanya hilo tayari."

"Yeye alijeruhiwa kwa maovu yetu; kwa kupigwa Kwake tumepona." Yeye hawezi kufanya hilo mara ya pili. Hivyo, unaona, Yeye amekwishafanya hilo tayari. Unapaswa uliamini. Hakuna lolote unaloweza kufanya, unastahili chochote, ku-kupata wokovu au uponyaji wako. Hakuna lolote unaloweza kufanya juu ya hilo. Ni kipawa cha bure cha Mungu. Unaona, ni neema, karama ya bure. Kama nikikupa dola milioni moja na uinyooshe tai yangu; sikukupa hizo; umefanya kitu fulani kwa ajili ya hizo. Unaona? Karama ya Mungu ni bure. Kitu pekee unachopaswa kufanya ni kuiamini hiyo, kwamba Yeye amenunua hii kwa ajili yako, wewe. Yeye… Imekwishanunuliwa tayari. Yeye alifanya hilo kwa ajili yako.

Na hakuna mtu ulimwenguni...

51 Mimi sijui umekuwa na nini hapa katika Baton Rouge. Kila kitu kinaingia polepole nchini, uigizaji na hilo. Tunajua hilo linapasa tu kuwa hivyo. Lakini mtu aingiapo na kukuambia yeye anao uwezo wa kukuponya, yeye anadanganya.

Mungu pekee anaweza kuponya. "Mimi ni Bwana nikuponyae magonjwa yako yote." Yeye hawezi kushirikiana utukufu Wake na mtu yeyote. Hakuna mtu aliye na uwezo wa kuponya. Lakini kuna mtu aliye na vipawa, kumdhihirisha Mungu. Mchungaji wako… [Ndugu Branhama anakohoa-Mh.] Samahani. Yeye anaweza kumchukua Mungu, kwa njia ya karama ya-ya… Mwalimu, anaweza kuelezea Neno hivyo ni lazima ulione Hilo. Kama una macho yoyote ya kuonea, utaliona. Kuna mwingine, labda karama fulani nyingine. Lakini siku zote kuna karama inayodhihirisha Uwepo wa Mungu, na, kupitia pale, wewe mwenyewe unapaswa kuiamini hiyo.

52 Mwenye dhambi anaweza kuja hapa madhabahuni kama kijana mwanamume au mwanamke, kwenye umri wa miaka kumi na nne, nao wangekuletea wewe chakula chako hapa, na ungemlilia Bwana, hadi ufikie umri wa miaka tisini, kamwe usingeokolewa. Lakini unapaswa kwanza ukubali kile Yeye alichofanya kwa ajili yako. Unaona? Unapaswa ukikubali hicho, mwenyewe. Kisha unapokikubali, ndipo Yeye anakuwa Kuhani Mkuu, mpatanishi, ili kufanya maombi juu ya ukiri wa kile unachokiamini. Sasa hilo ni jambo lile lile kwa karama namna hii. Ni kuondoa akili yako kwako, na kisha uone kile Yeye anachosema ufanye.

53 Nawaona watu wakija jukwaani, wanaruka juu na chini na kupiga kelele, na kusema, "Loo, Ndugu Branham, ninayo imani yote ulimwenguni." Unafanya nini hapa, basi? Unaona? Huo ni-huo ni msisimko, siyo imani. Imani halisi haijui kushindwa. Limekwishafanyika tayari. Limekwisha tayari. Mungu alisema hivyo, na hilo linamaliza hilo, unaona. "Mungu alisema hivyo!"

Sasa ni kitu kile kile, wakati wowote. Unapoamini hilo kwa kweli, hilo linamgusa Yeye. Sasa yule mwanamke mdogo aliyegusa vazi lake, yeye alisema, "Kama mimi nitagusa tu vazi lake, nitafanywa kuwa mzima," naye alilifanya hilo. Na yeye alitimiza kile imani yake ilichotaka yeye afanye, "kugusa hilo," Yeye alihisi hilo, unaona, na Yeye

akageuka na kunena naye. Sasa, Yeye ni yule jana, leo, na hata milele. Kama utamwamini tu Kristo, umwamini Yeye! Hebu imani yako iguse vazi lake.

Na Yeye, sasa hivi, ni Kuhani Mkuu awezaye kuguswa na hisia za madhaifu yetu. Sote tunajua hilo. Na kama Yeye ni yule jana, leo, na hata milele, itampasa Yeye atende leo kama alivyotenda jana kama Yeye ni Kuhani Mkuu yule yule. Sasa hutaamini hilo? Uwe tu na imani katika Mungu.

54 Kama nimewaambia uongo, basi Mungu hatausaidia. [Sehemu tupu kwenye kanda-Mh.] ... juu yangu, kama hayo hayanishuhudii mimi, basi msiliamini hilo," mnaona. Na kama Maandiko hayashuhudii kile ninachowaambia sasa, kwamba, "Yeye ni yule jana, leo, na hata milele," basi msiamini Maandiko. Kwa sababu, Andiko lilisema Yeye alikuwa. Na Yeye aliahidi haya mambo kwa ajili ya kipindi hiki cha mwisho.

Kumbukeni, penye mwisho tu wa kipindi cha Kiyahudi, hivyo ndivyo anavyojifunua Mwenyewe, Masihi. Mwisho wa-wa kipindi cha Wasamaria, Yeye alifanya hivyo hivyo. Sasa ni mwisho wa kipindi cha Mataifa. Yeye ni yule jana, leo, na hata milele. Mwamshe Yeye katika dhamiri yako, mwite Yeye penye sehemu ya tukio, tunapoinamisha vichwa vyetu.

55 Baba wa Mbinguni, neno moja kutoka Kwako litatosheleza. Hilo litakuwa tu yote tunayohitaji, neno moja tu kutoka Kwako. Hebu watu waelewe kwa wazi ni mafanikio gani,kile tunachojaribu kufanya, Bwana, ni ku-ni kuwaruhusu wao wapate manufaa ya Bwana Yesu wanayempenda na kumtumikia. Hebu wao wafanye hilo jioni hii, Bwana. Kwa sababu, mauti yako haikuwa bure. "Ulijeruhiwa kwa ajili ya makosa yetu, ukachubuliwa kwa ajili ya uovu wetu." "Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake, na kwa kupigwa Kwake sisi tumepona."

Naomba, Mungu, kuwa kila mmoja ndani hapa, katika Uwepo wa Kiungu, atafahamu hili na atapata ono, na ataponywa kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Kupitia Jina la Yesu Kristo, najileta mwenyewe pamoja na hili kusanyiko, kwa heshima na utukufu Wake. Amina.

56 Sasa mmwe wanyenyekevu hasa, kwa dakika chache tu. Sasa neno moja tu kutoka Kwake litamaanisha zaidi kuliko yote niwezayo kusema, au yote yeyote angeweza kusema, kwa sababu ni Yeye akilifanya hilo. Yeye ndiye. Yeye ndiye mtendaji, ba sisi tunatumaini kwamba Bwana Yesu atatujalia haya mambo kwenu.

Sasa, kila mmoja... Sasa, hebu tuone ni wakati gani.Sikujua ilikuwa huo. Nawaambieni, tutatoka nje hapa kwa wakati, kile tunachopaswa, hatuna wakati wa kuleta huu mstari. Hebu tuite moja kwa moja kutoka kwenye mkutano.

57 Sasa hebu tuchukue tu Andiko, kwa dakika moja tu. Sasa Biblia inaahidi, katika siku hii, kwamba kurudia kwa Sodoma na Gomora kutarudiwa. Ni wangapi wanaamini hilo sasa, uinue mkono wako? Biblia inafananishwa na hilo sasa. Na kisha kilikuwa nini hicho kule Sodoma na Gomora? Ilikuwa ni Mungu katika umbo la mwanadamu. Na kwa namna ambayo Abrahamu alilijua hilo, ni wakati Yeye aliposema, "Kwa nini Sara amecheka katika hema, nyuma? Au, kwa nini yeye alilitilia shaka hilo, yale maneno Yeye aliyonena kuwa yangekuwa?" Yeye aliweza kutambua kile Sara alichokuwa akiwaza, nyuma Yake. Sasa uone tu kama haikuwa hivyo.

Sasa, hilo halikuwa kwa kanisa la Babeli, au kanisa la Sodoma. Hapana, hapana. Hilo halikuwa kwa hao watu chini kule katika matabaka ya kidhehebu. Hapana, bwana, kamwe haliendi kwao. Wao wanaye mjumbe wao. Unaona? Lakini kwa Kanisa teule, ule Uzao mkuu wa Abrahamu unaopaswa kuamini Neno pasipo kujali hali iko vipi, "Abrahamu aliyaita hayo mambo kana kwamba yalikuwako." Mungu alisema hivyo, na yeye aliamini hilo. Sasa, rafiki, na-najua kuwa Mungu anawajibika kwa hili Neno, kulitimiza.

58 Sasa nataka, kokote uliko katika jengo, kukaa kwa unyenyekevu kwa kitambo kidogo, popote ulipo. Na amini, amini kwa moyo wako wote.

Sasa kama ningeweza kukuponya wewe, kama ningeweza kumponya huyu msichana mdogo ambaye moyo wangu unatoka kwa ajili yake, kama ningeweza kumponya kile kitu kidogo kilicholala pale, ni-ni-ninge-ningetambaa kutokea hapa kwenda Ncha ya Kaskazini, kama ningeweza, ili kufanya hilo. Mtu yeyote aliye na hisia ya kibinadamu... Lakini singeweza kufanya chochote.

Labda baadhi yenu kule hamtaishi isipokuwa kidogo, kwa saratani. Kama

ningeweza kuwaponya, ningekuwa…Nisingefaa kusimama katika hili jukwaa kama ningeweza kufanya hilo na ningefanya hilo. Sasa, singeweza. Moyo wangu unajihusisha na ninyi. Mimi ningelifanya hilo kama ningeweza, lakini siwezi. Hakuna mtu mwingine awezaye kufanya hilo. Hilo ni sahihi.

Lakini mnaona, Yesu amekwishalifanya hilo. Mnaona? Na Yeye anajaribu tu kukufanya wewe uamni hilo. Lakini wewe...

59 Lakini nawasikitikia watu. Kumekuweko na mambo mengi yaliyowapofusha tu, namna hii na namna ile, hadi, watu masikini, kama kondoo wasio na mchungaji, mara chache. Wao hawajui la kufanya. Mmoja anasema hili na mmoja anasema lile.

Usiwaze kile mtu alichosema. "Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama hiki kama ubatizo wa Roho Mtakatifu." Na, kumbukeni, Petro alisema, penye siku ya Pentekoste, "Ahadi ni kwa ajili yenu na kwa watoto wenu, na kwa hao walio mbali, na watatakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie," Mnaona.

Yesu aliahidi haya mambo yangelitokea katika siku za mwisho, kwamba Mungu angerudi katika umbo la mwili wa mwanadamu, kama wewe na mimi hapa jioni hii, na angetenda jambo lile lile kabla tu ulimwengu haujaangamizwa. Na ulimwengu ungekuwa kama Sodoma. Mnaona? Sasa tunayo hali ya Sodoma sawasawa; kila mahali pake, kila mtu pekee, kila kitu kikiwa kimewekwa sawasawa kabisa.

Sasa, imani yetu haiwezi kuja kwenye hilo? Je, hatuwezi kumwita Yeye kwenye sehemu ya tukio? Mwiteni kwenye sehemu ya tukio. Imani yako ndicho kitu pekee kinachoweza kufanya hilo. Sasa amini kwa moyo wako wote, kila mmoja wenu sasa.

60 Na nataka kuwaomba jambo fulani. Pasipo kadi yoyote ya maombi,… -sipo mtu yeyote juu hapa, kama huyo Roho Mtakatifu mkuu atashuka chini hapa, na kwa njia ya upako wako na upako juu yangu, na atatambulisha kuwa Yesu Kristo anatenda kazi miongoni mwetu namna hii, Yeye angefanya nini zaidi? Hakuna ahadi nyingine katika Biblia, zaidi ya hiyo. Hiyo ndiyo ahadi kuu. Ni wangapi wanajua hilo? Hakika ni hiyo. Ni-ni kitu cha mwisho kwa kipindi cha kanisa.

Wayahudi, katika wakati wa kipindi cha Dhiki, na kwenye…kule wao walikuwa na-na ujio nyuma kule, lakini siyo kanisa la Mataifa. Hiki ni kitu cha mwisho kilichoahidiwa kwa Mataifa. Ni kweli. Unaona, ilikuwa ni Mataifa chini kule katika Sodoma, ulikuwa unakwenda kuteketezwa. Na hilo, hapa katika Bi-Bibiarusi, ambaye alikuwa Uzao wa Kifalme wa Abrahamu, akiwa Bibiarusi aliyeitwa atoke miongoni mwa Mataifa. Hiyo ndiyo ishara yao ya mwisho, lote la hilo.

61 Liwekee alama katika kitabu chako. Mimi ni mzee. Lakini liwekee tu alama katika kitabu chako na uone kama litatukia, ama la, unaona.

Mko mwishoni sasa. Lini? Mimi sijui. Namtazamia Yeye leo. Kama Yeye hayupo hapa leo, nitamtarajia Yeye kesho. Kama yeye hayupo hapa kesho, nitamtarajia siku inayofuata. Kama Yeye hayupo hapa mwaka huu, nitamtarajia Yeye mwaka ujao. Najua Yeye anakuja. Mimi sijui dakika au saa, lakini najua kila kitu kimetimia, tayari kwa ajili ya Unyakuo. Kanisa limeitwa. Itakuwa ni kuondoka kwa siri; kutoweka tu, na hilo litakuwa limekwisha.

Na ulimwengu utaendelea tu kama kawaida, watu wakihubiri, na watu wakifikiri wanaokolewa, kabisa tu kama walivyofanya katika siku za Nuhu, na kadhalika. Nuhu aliingia katika safina, na watu waliendelea, na ulimwengu ukigeuka kama kawaida. Wazia hilo! Na, wakapotea Milele, wakifikiri wameokolewa.

62 Baadhi ya hizi siku nakwenda kuleta hema kubwa katika nchi hii, na kuliweka juu hapa, hivyo tuweze kuwa na ibada za alasiri, na maelekezo, ili muweze kufahamu haya mambo vizuri zaidi. Tuwe na ndugu zetu wote pamoja ili tuweze kuwa na ibada.

Sasa kama Yesu Kristo anatimiza ahadi Yake, basi sisi tunawajibika kumwamini Yeye. Nawatakeni nyote, kila mmoja wenu, kuwa tu na imani rahisi tu kama ya mtoto, kumwamini Yeye.

Sasa kama ambavyo ni namna ya kuanza mkiwa mmeinamisha vichwa vyenu, na kuanza kuomba, mkisema, "Bwana Yesu, sasa najua kuwa huyu mtu hanijui mimi. Nami ni mhitaji. Na tunaambiwa kuwa Wewe ni Kuhani Mkuu unayeweza kuguswa na hisia za madhaifu yetu. Kama tu Wewe utamruhusu yeye… Kama ninaweza kukugusa Wewe, nena tu kupitia yeye, Bwana, kwamba nita, najua ninii… najua ni Wewe. Najua yeye

anifahamu mimi.”

Na hilo kule katika mkutano, kusanyiko tu lililochanganyikana; la kuamini, kutokuamini, kujifanya kuamini; wenye dhambi, watakatifu, na wote pamoja.

63 Sasa ni lazima uamini.

Sasa kama Yeye atafanya hili kutokea hili kusanyiko hapa... nataka kila mmoja wenu ndani hapa, aseme, “Ndugu Branham, najua kuwa huyo inapasa awe Yeye,” anayetazamia juu ya kusanyiko kama Yeye alivyofanya wakati ule.

Nawatakeni... kama kwa kweli mtaamini, nataka uinue mkono wako, useme, “Bwana, nitalikubali hilo kwa moyo wangu wote, kwamba naamini ni Kristo Yesu, kulingana na ahadi yake.” Kote kwenye jengo. Mungu awabariki. Hilo ni zuri. Ee, ni vibaya tu sana hatuna mwezi wa kuwa hapa. Unaona, tuwe tu…Mimi ni mgeni kwenu. Mnaona, ni vigumu. Endelee tu kuamini.

Sasa, ni Nuru. Mungu ni Nuru, tunajua hilo, Nguzo ya Moto. Na sasa muombe tu na kuigusa Hiyo, na hebu Bwana Yesu ajibu.

Sasa nachukua kila roho hapa chini ya udhibiti wangu, katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya utukufu Wake. Sasa mmwe wanyenyekevu hasa. Ombeni. Mmwe wanyenyekevu hasa.

64 Sasa, Hii hapa. Kuna bibiye hapa mbele yangu. Yeye ameinamisha kichwa chake, naye anaomba kwa ajili ya mateso yake mwenyewe. Kama unataka kuinua kichwa chako sasa, yeye yupo papa hapa mbele yangu. Je, unaamini kwa moyo wako wote? Je, unaamini kuwa Mungu anaweza kuponya kisukari na kukufanya uwe mzima? Sasa, hiki ndicho kisukari.

Mimi sikujui wewe. Wewe ni mgeni kabisa kwangu. Lakini je unaniamini mimi kuwa mtumishi Wake? Kama-kama sisi ni wageni mmoja kwa mwingine, inua mkono wako, namna hiyo, ili watu waone. Unaona? Vema. Unaona, hapa kuna bibiye. Na sasa yeye anaumwa hali ya ugonjwa wa kisukari. Na unaamini kuwa Mungu anaweza kuniambia wewe ni nani? Je, hilo litakufanya uamni? Wewe ni Bibi Martin. Kama hilo ni sahihi, inua mkono wako. Unaona? Uwe tu na imani. Usitie shaka. Uwe na imani.

Sasa yeye aligusa nini? Nataka kuliuliza kusanyiko. Yeye aligusa nini? Huyo hapo mwanamke akiwa ameinua juu mkono wake wa kuume, na wa kwangu, pia, mbele za Mungu. Mnaona? Yeye aligusa kitu Fulani. Mwanamke mdogo wa kawaida tu, kwa kweli hilo, kuwaambia ukweli, sasa mnaona kama hili ni kweli, lilimshangaza yeye. Yeye hakujua kuwa alikuwa na imani kiasi hicho. Imani siyo kitu fulani unachokitengeneza; ni kitu fulani ulicho nacho. Mnaona? Yeye alishangaa. Hata hivi sasa huyo mwanamke anajisikia tofauti kuliko alivyokuwa dakika chache zilizopita. Yeye anajua kitu fulani kilimtokea.

65 Hapa, je, hamwoni hiyo Nuru? Sawa. Hamuioni Hiyo papa hapa juu ya huyu mwanamke papa hapa, pale pale nyuma? Yeye anaugua… Yeye ameinamisha kichwa chake. Anaomba. Lakini anaumwa na tatizo la mgongo wake. Kama yeye ataamini kwa moyo wake wote, anaweza kupona hilo tatizo la mgongo. Hakika. Yeye anakwenda kulikosa hilo, hakika tu kama chochote. Ona, maombi yake bado yanaendelea. Bwana, nisaidie. Bibi. DeVille, ni wewe.

Hiyo ni neema. Huyo mwanamke alikuwa anaomba, hata hakuwa anawaza, hata hakunisikia mimi nikisema lolote. Sasa mwulize yeye kama ananifahamu mimi. Ndiye huyo, na hilo ndilo tatizo lake. Hivyo yeye aligusa nini? Huo ni uthibitisho wa Yesu Kristo, Neno, hutambua mawazo yaliyoko moyoni.

66 Je, mnaamini? Iweni na imani tu. Ombeni, kokote. Aminini tu. Ni hilo tu mpasalo kufanya. Aminini tu, aminini nimewaambia ile Kweli. Sasa, mimi siyo Yeye. Mimi ni mtumishi Wake tu, mtumishi Wake tu.

Kama tu mtakuwa na imani ya kutosha! Siwezi kumwita yeye. Najua tatizo lake, lakini, mnaona, nasubiri tu kidogo na huenda litabadilika. Hakika siyo haiwezekani, lakini unapaswa utoke kwenye kwenye hicho kifungo. Yeye hawezi kuamini binafsi. Unapaswa uamini kwa niaba yake.

Bibiye mmoja anaumwa tatizo la figo. Yeye hatokei hapa. Yeye anatokea Mississippi. Yeye ataamini kwa moyo wake wote, Mungu ataponya hilo tatizo la figo. Bibi Palmer, kama utaamini kwa moyo wako wote, unaweza kuponywa hilo. Hilo limekwisha

kumwachilia. Nuru iligeuziwa juu yake. Imeondoka kwake. Uwe na imani katika Mungu. Usitie shaka.

67 Kuna bibiye aliyeketi hapo hapo kando yake. Yeye anaumwa na baridi yabisi. Je, unaniamini mimi kuwa nabii wa Mungu, bibiye? Unaniamini? Unaamini kama Mungu ataniambia wewe ni nani, hilo litakusaidia kuamini? Jina lako ni Bibi Meadow. Amini kwa moyo wako wote sasa, unaweza kupona, pia.

Hilo lilipata moto kwa bibiye aliye karibu naye. Yeye ameketi pale, pia. Hiyo inakwenda pale, moja kwa moja chini kwenye mstari. Bibiye aliyeketi pale, yeye anaumwa na... Karibu naye, anaumwa na kisukari, ugonjwa wa sukari. Wao wanamtaka aende hospitali, lakini anakataa kufanya hilo. Yeye ana mwanawe anayemwombea, pia. Huyo mwana hayupo hapa, lakini unaamini Mungu anaweza kuniambia wewe ni nani? Bibi Dufflee, D-u-f-f-e-e, namna hiyo. Hilo ni sahihi. Je, hilo ni sahihi, inua juu mkono wako, kwa mikono yako juu. Vema. Sasa uamini, na naweza kufanywa mzima, pia.

68 Je, unaamini kuwa hicho ni kitu kile kile ambacho huyo... Je, unaamini kuwa Uwepo wa Yesu Kristo upo hapa sasa? Ni wangapi wanalikubali hilo? Loo, ni usalama ulioje! Ni usalama ulioje!

Mnaona, mlifanya nini? Mlimwamsha Yeye. Mlimlete Yeye kwenye sehemu ya tukio. Yeye yupo hapa kwenye sehemu ya tukio. Hilo halifanyi tofauti yoyote mitumbwi inasema nini. Kumbukeni, yeye anaweza kusema, "Nyamaza, tulia." Je, unaliamini hilo kwa moyo wako wote?[Kusanyiko linashangilia na kusema, "Amina."-Mh.] Kama unaamini, simama juu kwa miguu yako na ulikubali hilo. Simama juu na useme, "Naamini hilo kwa moyo wangu wote." Inuka juu kwa miguu yako. "Najua naamini." Hilo ni sahihi, haidhuru shida yako ni nini, simama juu, mpe Yeye Sifa.

Baba wa Mbinguni, tunakuletea huu mkutano. Wao wanatambua kuwa Wewe upo hapa, Bwana. Hebu kila pepo, kutokuamini, hebu uondoe mkono wake, na hebu Yesu Kristo uliponye hili kusanyiko. Shetani, toka kwenye hadhara hii! Katika Jina la Yesu Kristo, unachukiwa.

MESSAGE hub online

www.messagehub.info

Mahubiri Na
William Marrion Branham
*"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7*